

**ASIYESIKIA LA MKUU, HUVUNJIKI GUU:**

1. SI KABANI AMENENA, SI MAMBO NA KUJUANA.  
KIVUMBI KIKIUMANA, SAHAU MAMBO KIJANA.  
MUDA SI KUNGOJEANA, VITUKO NA KUTISHANA.  
**WAKUU WAKISHASEMA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
2. WA UNDUGU WETU NDUGU, BUSARA MEJAZA CHUNGU.  
WAMEUTOA UKUNGU, MEBAKI WEWE MWENZANGU.  
UKWELI MWIBA UTUNGU, MAISHA NI KWANGU KWANGU.  
**WAKUU WAKISHASEMA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
3. SISEME MATSI NI NGUMU, KUPITA JUE MUHIMU.  
WENGINE KEMIA SUMU, SISHIKI HATA KWA NDIMU,  
NDO MWANZO WAJIHUKUMU, KUJIAMINI MUHIMU.  
**WAKUU WAKISHASEMA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
4. SIKUHADAE KAMANDA, MUISAKATE KANDANDA.  
TASHINDWA FUNGA MKANDA, YO MIMBA IKIKUGANDA!  
WACHA AKWITE KINANDA, LAKINI SIMPE TUNDA.  
**WAKUU WAKISHANENA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
5. KATAKA UDAKITARI, FIKIRI KIDAKITARI.  
WAUTAKA URUBANI, YAJUE YAKO ANGANI.  
LENGO UUNDE INJINI, ANZA YAKITABUNI.  
**WAKUU WAKISHANENA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
6. SIACHE SOMA VITABU, MASWALI YANA MAJIBU.  
ULIZA SONE AIBU, MWALIMU ATAKUJIBU.  
KINYAMAZA KAMA BUBU, TAJILAUMU SULUBU.  
**WAVYELE WAKISHASEMA, SIKIA SIVUNJE GUU.**
7. SAFARI BADO NI NDEFU, USIJISIFU KWA NDEVU.  
WAZAZI UWAKASHIFU, HATA NYANI ANA SHAVU.  
NIDHAMU KIWA PUNGUFU, TAYAPATA MAUMIVU.  
**WAKISHASEMA WAVYELE, SIKIA SIVUNJE GUU.**
8. NATAMATISHA MALENGA, MBELE NATAKA KULENGA.  
AKILI IMENIGONGA, NIENDELEE KULONGA.  
SIMDHARAU MKUNGA, 'KWELI WEUPE WA UNGA.  
**UNDUGU WAKISHANENA, SIKIA SIVUNJE GUU.**

Na: Kabani Stephen (mcJibe)

Rununu: 072194884.

stephenkabani@yahoo.com 15<sup>TH</sup> JUNE 2013.